



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA KAKONKO

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)

Simu Na. +255 (028) 2988881

S.L.P. 03,

Fax Na. +255(028) 2988881

KAKONKO.

E-mail: ded@kakonkocd.go.tz

Tovuti : www.kakonkocd.go.tz

Unapojibu tafadhali taja

Tarehe 23.07.2022

TANGAZO -MARUDIO

UUZAJI WA MAGARI CHAKAVU KWA NJIA YA MNADA

MWALIKO WA MNADA WA HADHARA

Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko imepata Kibali kutoka kwa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango cha kuuza Magari chakavu kwa njia ya mnada wa hadhara kama ilivyoainishwa hapa chini:-

MAGARI

SN	AINA YA MTAMBO	NAMBA YA USAJILI	HALI YA KIFAA	MAHALI ILIPO
1	GARI TOYOTA LANDCRUSER GX	SM 4430	HALITEMBEI/ GROUNDED	OFISI YA ZAMANI YA H/WILAYA KAKONKO
2	TOYOTA HILUX	DFP 3298	HALITEMBEI/ GROUNDED	OFISI YA ZAMANI YA H/WILAYA KAKONKO
3	LANDROVER 110 TDI AMBULANCE	DFP 2494	HALITEMBEI/ GROUNDED	KITUO CHA AFYA KAKONKO

MASHARTI YA MNADA:

1. Mnunuzi atatakiwa kulipa asilimia 25% siku hiyohiyo ya mnada na kiasi kilichobaki kilipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Endapo Mnunuzi atashindwa kulipa ndani ya muda huo basi kiasi kilichotolewa cha asilimia 25% hakitarudishwa na Mnada utarudiwa tena.
2. Mtu yeyote atakayetamka bei ya juu kisha akashindwa kulipa asilimia 25% ya bei aliyotamka atachukuliwa kuwa ni mwenye kutaka kuvuruga mnada na hivyo hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake kwa mjibu wa sheria ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
3. Ukaguzi utanza mara baada ya tangazo hili kutolewa ambapo ukaguzi utafanyika saa za kazi kuanzi tarehe 4-5/8/2022 saa 1:30 asubuhi hadi saa 9:30 mchana.
4. Gharama ya ubadilishaji hati ya Umiliki ni ya mteja hasa kwa vyombo vya moto kama vile magari na kutakiwa kubadilisha ndani ya siku 21.
5. Mnunuzi atatakiwa kuondoa/kuchukua chombo alichonunua ndani ya siku 7 kuanzia siku ya kukamilisha malipo.
6. Vifaa vitauzwa kwa kuzingatia hali iliyopo hivyo Halmashauri haitahusika na matengenezo yoyote.

TAREHE NA ENEO LA MNADA

Mnada utafanyika tarehe 06/08/2022 siku ya Jumamosi kuanzia saa nne asubuhi hadi saa nane (8:00) mchana katika Ofisi za zamani za Halmashauri ya Wilaya ya kakonko.

Wananchi wote mnakaribishwa.



Michael S. Faraay
KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA
KAKONKO